


# SPACE SCOOP

Bringing news from across the Universe to kids all around the world



EU UNIVERSE  
AWARENESS

## Uvumbuzi wa Sukari Angani



Je ulikuwa unafahamu kuwa sukari ina vimelea muhimu vya uhai? Ingawa hii haimaanishi kuwa kula vitu vitamu kwa wingi ni kuongeza uhai. Sukari imetengenezwa kwa fomula rahisi iliyo tokanana na kemikali ziitwazo carbon, hydrogen na oxygen. Kemikali hizi ndizo zilizojenga karibu kila mwili wa kiumbe hai anayepatika hapa duniani pamoja na kemikali nyingine ya nitrogen.

Hivyo basi timu ya wanaastronomia kwa kutumia telescope yenye nguvu wameweza kuona sukari kwenye gesi zinazopatikana kuzunguka nyota ndogo yenye ukubwa sawa na Jua letu. Sukari ilishawahi kuonekana angani, lakini hii ni mara ya kwanza kuonekana kwa ukaribu katika nyota inayofanana na Jua. (Umbali uliopo katika ya sukari hii na jua ni sawa na umbali uliopo katika ya Jua na sayari ya Uranusi). Na kwa vile sukari ina vimelea vya maisha, kuonekana kwake karibu na nyota inayofanana na jua ni habari nzuri sana. Kitu ambacho kinaonyesha kuwa maisha kama yetu yanawezekana kupatikana katika sayari nyingine ulimwenguni!

Wanaanga hawa wamegundua pia, sukari hii huingia ndani kuelekea katika nyota. "Sukari hii siyo tu kwamba ipo katika sehemu sahihi ya kuweza kuingia kwenye sayari, lakini pia inasogea kuelekea katika ulekeo sahihi" anasema mwanaastronomia Cécile Favre.

Jihusishe: Je ni kitu gani ungeweza kukigundua kama ungekuwa unashughulika na moja katika ya telescope kubwa zaidi Duniani? Papo hapo ili kusheherekea miaka 50 ya Kituo cha Anga cha Ulaya Kusini unaombwa kupiga kura juu ya kitu umbacho ungependa kichunguzwe na telescope yake kubwa iitwayo VLT! Bofya hapa kwa faarifa zaidi



More information about EU-UNAWE  
Space Scoop: [www.eu-unawe.org/kids/](http://www.eu-unawe.org/kids/)